**JIMBO LA MAINE**

# MTOA HUDUMA ZA UTUNZAJI WA WATOTO
# (VITUO VYA UTUNZAJI WA WATOTO NA WATOA HUDUMA ZA UTUNZAJI WA WATOTO)
# KANUNI YA KUTOA LESENI YA UKAGUZI WA HISTORIA

**10-148 KANUNI YA SHERIA ZA MAINE**
**SURA YA 34**

**Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu ya Maine**
**Ofisi ya Huduma za Watoto na Familia**
**11 State House Station**
**Augusta, Maine 04333-0111**

**Itatekelezwa**
**Tarehe 12 Mei, 2022**

# Jedwali la Yaliyomo

**SEHEMU YA 1. KAULI YA MADHUMUNI ........................................................................ 1**
**SEHEMU YA 2. FASILI ........................................................................................................ 2**
**SEHEMU YA 3. UCHUNGUZI WA HISTORIA ....................................................................... 4**
A. Watu wanaofanyiwa ukaguzi wa kina wa historia kubaini uhalifu. ................................ 4
B. Watu ambao hawafanyiwi ukaguzi wa kina wa historia kubaini uhalifu. ........................ 4
C. Watu wanaobadilisha ajira. ........................................................................................ 4
D. Vipengele vya ukaguzi wa kina wa historia. ................................................................ 4
E. Mchakato unahitajika. ................................................................................................ 4
F. Marudio ..................................................................................................................... 5
G. Barua ya Ustahiki. ..................................................................................................... 5
H. Haki za Kukata Rufaa. ................................................................................................ 5
I. Faragha. ...................................................................................................................... 5
J. Kutostahiki kwa Ajira. ................................................................................................. 5
K. Wajibu wa Mtoa Huduma ya Utunzaji wa Watoto. ........................................................ 6
L. Kukatazwa Leseni. ..................................................................................................... 6
M. Uchunguzi wa historia wa hiari .................................................................................. 6
**SEHEMU YA 4. MCHAKATO WA RUFAA NA HAKI ........................................................... 7**
A. Usahihi Halisi wa Taarifa ............................................................................................ 7
B. Uthibitishaji wa Unyanyasaji au Utelekezaji wa Watoto. ............................................... 7
C. Kuhukumiwa kwa sababu ya kosa. ............................................................................. 7
**MAMLAKA YA UONGOZI NA HISTORIA YA UDHIBITI……………………………...8**

**10-148 C.M.R. Sura ya 34**

**Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu**
**Ofisi ya Huduma za Watoto na Familia**

# KANUNI YA KUTOA LESENI YA UKAGUZI WA HISTORIA YA WATOA HUDUMA YA UTUNZAJI WA WATOTO (VITUO VYA UTUNZAJI WA WATOTO NA FAMILIA AMBAZO NI WATUNZAJI WA WATOTO)

---

## KAULI YA MUHTASARI

Sheria hii imewekwa ili kudhibiti ukaguzi kamili wa uhalifu kwa watoa huduma za watoto walio na leseni (ambayo ni pamoja na vituo vya utunzaji wa watoto na familia ambazo ni watunzaji wa watoto) kwa mujibu wa masharti ya 22 M.R.S. § 8302-A na § 8302-C na 42 USC § 9858f (b) na kulinda afya, usalama na ustawi wa Watoto wanaohudumiwa.

---

## MAMLAKA

Sheria hii imetangazwa chini ya mamlaka ya 22 M.R.S. §§ 42(1) na 8302-A(1)(J),(2)(K).

**KANUNI HII INA TAREHE YA KUTUMIKA KISHERIA YA 25 SEPTEMBA, 2021**

**KANUNI HII INA TAREHE YA KUTUMIKA KISHERIA YA 25 SEPTEMBA, 2021**

## SEHEMU YA 1. KAULI YA MADHUMUNI

**A. Kauli ya Madhumuni**. Madhumuni ya sheria hii ni kuweka viwango kamili vya kutoa leseni za ukaguzi wa historia kwa Watoa Huduma za Utunzaji wa Watoto (ambavyo vinajumuisha vituo vya utunzaji wa watoto na familia ambazo ni watunzaji). Kanuni hii inaanza kutekelezwa kwa mujibu wa 22 M.R.S. §§ 8301-A(8), 8302-A (1)(J),(2)(K), na 8302-C na inaelezea masharti ya ukaguzi wa kina wa historia na mchakato wa kukata rufaa kwa masharti mahususi ya kutostahiki.

**B. Kanuni hii ina tarehe ya kutumika kisheria ya 25 Septemba, 2021.**

## SEHEMU YA 2. FASILI

**A. Fasili.** Kama inavyotumika katika kanuni hii, isipokuwa muktadha ukionyesha vinginevyo, maneno yafuatayo yana maana zifuatazo:

1. **Dhuluma au Kutelekezwa** ni tishio la afya au ustawi wa Mtoto kutokana na majeraha au uharibifu wa kimwili, kiakili au kihisia, unyanyasaji au dhuluma ya kingono, kunyimwa mahitaji muhimu au kukosa kulindwa dhidi ya mambo haya, ambayo yanafanywa na mtu anayewajibikia Mtoto.

2. **Mtu mzima** ni mtu wa umri wa miaka 18 na zaidi.

3. **Mtoa Huduma za Utunzaji wa Watoto** inamaanisha nyumba au mahali pengine ambapo mtu hutunza au kutekeleza mpango ulioratibiwa kufanywa mara kwa mara, kwa sehemu yoyote ya siku, kutoa utunzaji na ulinzi kwa watoto watatu au zaidi wa umri wa kati ya wiki 6 na miaka 12, au mtu anayetoa utunzaji wa watoto. Watoa Huduma za Utunzaji wa Watoto hutoa huduma hii kwa watoto ambao si watoto wa Mtoa Huduma za Utunzaji wa Watoto au ambao hawaishi katika nyumba ya Mtoa Huduma za Utunzaji wa Watoto, kwa ajili ya mazingatio.

   **a.** Mtoa Huduma ya Utunzaji wa Watoto ni pamoja na:

      **i.** Mpango unaoendeshwa katika makazi ya kibinafsi, unaowatunza watoto 3-12, kama inavyofafanuliwa katika 22 M.R.S. § 8301-A(1-A)(C) ("Familia Inayotoa Utunzaji wa Watoto");

      **ii.** Mpango unaoendeshwa katika jengo linalomilikiwa au kukodishwa na Mtoa Huduma ya Utunzaji wa Watoto, unaowahudumia watoto 3 au zaidi, kama inavyofafanuliwa katika 22 M.R.S. § 8301-A(1-A)(B) ("Taasisi ya Utunzaji wa Watoto") na 22 M.R.S. § 8301-A(1-A)(E) ("Kituo Kidogo cha Utunzaji wa Watoto"), kinachojulikana kama Kituo cha Utunzaji wa Watoto; na

      **iii.** Mpango unaowahudumia watoto wa umri wa kati ya miezi 33 na miaka 8, kwa kipindi kisichozidi saa tatu na nusu, kama inavyofafanuliwa katika 22 MRS § 8301-A (1-A)(D) ("Shule ya Chekechea").

   **b.** Mtoa Huduma ya Utunzaji wa Watoto haijumuishi:

      **i.** Kambi ya majira ya kiangazi ya makazi au ya usiku kucha iliyoanzishwa kwa madhumuni ya burudani na elimu pekee, iliyoidhinishwa kwa mujibu wa 10-144 CMR Sura ya 208, Kanuni Zinazohusiana na Kambi za Vijana, Kambi za Kimsingi na za Safari;

      **ii.** Mpango unaotoa maagizo mwafaka kwa Watoto kwa madhumuni ya kufundisha stadi moja kama vile karate, densi au mpira wa vikapu;

      **iii.** Shule ya kibinafsi inayotambuliwa na Idara ya Elimu kama mtoaji wa mafundisho ya usawa kwa madhumuni ya mahudhurio ya usawa ya shule; au

      **iv.** Shule rasmi ya umma au ya kibinafsi ya asili ya shule ya chekechea, msingi au sekondari iliyoidhinishwa na Kamishna wa Elimu kwa mujibu wa Kifungu cha 20-A.

4. **Barua ya Kustahiki kwa Mtoa Huduma ya Utunzaji wa Watoto** ni barua iliyotumwa na Idara kwa Mtoa Huduma ya Utunzaji wa Watoto kuhusu Mfanyakazi anayehudumu au Mfanyakazi mtarajiwa ambaye alihitajika kufanyiwa ukaguzi wa kina wa historia ambao unaripoti hali ya

kustahiki pekee, na hauonyeshi maelezo mahususi ya kutostahiki au maelezo yoyote ya siri kuhusu mtu binafsi anayefanyiwa ukaguzi wa kina wa historia.

5. **Idara** inamaanisha Ofisi ya Huduma za Watoto na Familia ndani ya Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu.

6. **Hitimisho** ni uamuzi uliofanywa na Idara kwa kuzingatia ukweli na ushahidi uliokusanywa wakati wa Uchunguzi ili kuegemeza uamuzi wa mtu anayewajibikia Mtoto, kwa kuzingatia ushahidi, kuhusu Mtoto aliyenyanyaswa au kutelekezwa.

7. **Mwanafamilia** ni mtu yeyote anayeishi katika nyumba ya Familia Inayotoa Huduma za Utunzaji wa Watoto au Mtoa Huduma za Watoto.

8. **Leseni** inamaanisha ruhusa iliyoandikwa, iwe ya muda, ya muda, ya masharti, au kamili, na Idara inayoidhinisha Mtoa Huduma za Utunzaji wa Watoto kufanya kazi. Kwa madhumuni ya sheria hii, Leseni ina maana sawa na "cheti" katika 22 MRS §8301-A.

9. **Mhudumu** ni mtu asiyehusiana na Watoto wote ambao wanapewa huduma za utunzaji ya watoto, ambaye ameajiriwa, au ametuma ombo la kuajiriwa na Mtoa Huduma kwa malipo (ikijumuisha wakandarasi huru) ambao shughuli zao zinahusisha utunzaji au usimamizi wa Watoto au ambao vinginevyo wana idhini ya kuwafikia Watoto bila usimamizi, ambao wanatunzwa au kusimamiwa na Mtoa Huduma za Utunzaji wa Watoto.

10. **Barua ya Mhudumu ya Kustahiki** ni barua iliyotumwa na Idara kwa mtu binafsi ambaye anfanyiwa ukaguzi wa kina (ikijumuisha Wanafamilia) ambayo inaripoti hali ya kustahiki, inatoa msingi wa uamuzi wakati mtu hajastahiki, na inatoa maelezo kuhusu haki ya mtu huyo kukata rufaa.

## SEHEMU YA 3. UCHUNGUZI WA HISTORIA

**A. Watu wanaofanyiwa ukaguzi wa kina wa historia kubaini uhalifu.** Kila Mtoa Huduma ya Utunzaji wa Watoto lazima aombe kufanyiwa uchunguzi wa kina wa uhalifu wao wenyewe, Wafanyakazi wote wa sasa na watarajiwa, Wanafamilia wote wa Familia Inayotoa Utunzaji wa Watoto, wa umri wa zaidi ya miaka kumi na minane, na watu wengine wowote ambao shughuli zao zinahusisha utunzaji au usimamizi wa Watoto au ambao wana idhini ya kuwafikia Watoto bila usimamizi wakiwa katika utunzaji wa Mtoa Huduma ya Utunzaji wa Watoto.

1. Ikiwa kuna hali chache ambapo mtu, mwenye umri wa miaka 18 au zaidi, anayeishi katika Familia Inayotoa Utunzaji wa Watoto hawezi kufanyiwa uchapishaji wa vidole, Idara inaweza kufanya ukaguzi wa kutumia jina wa historia ya uhalifu wa Jimbo na Shirikisho. Taarifa kutoka kwa mtoa huduma ya matibabu ya mtu binafsi lazima itolewe kwa Idara na ijumuishe taarifa ya jumla kuhusu hali ya mtu binafsi ambayo inazuia uwezo wa kuchukuliwa kwa alama za vidole. Hii inaweza kujumuisha kwamba mtu huyo anaishi nyumbani kwa sababu ya umri au ulemavu.

**B. Watu ambao hawafanyiwi ukaguzi wa kina wa historia kubaini uhalifu.** Watu ambao hawafanyiwi ukaguzi wa kina wa uhalifu wanaweza tu kuwa na ufikiaji unaosimamiwa wa watoto ambao wanatunzwa na mtoa huduma. Ukaguzi wa kina wa uhalifu hauhitajiki kwa watu ambao wana ufikiaji wa nadra unaosimamiwa wa watoto, ikijumuisha, lakini sio tu, wazazi, watu wanaosafirisha bidhaa, wakandarasi wanaofanya matengenezo na ukarabati na watu wanaoondoa taka.

**C. Watu wanaobadilisha ajira.** Mtu aliyefanyiwa ukaguzi wa uhalifu na kustahiki ambaye anatii sehemu hii, uliokamilishwa ndani ya miaka mitano iliyopita, na kwa sasa ameajiriwa kama Mfanyakazi au amekuwa ameajiriwa kama Mfanyakazi ndani ya siku 180 zilizopita hahitajiki kuomba ukaguzi mpya wa uhalifu anapotafuta ajira kwa Mtoa Huduma Tofauti wa Utunzaji wa Watoto.

**D. Vipengele vya ukaguzi wa kina wa historia.** Sajili, hifadhi na hifadhidata zifuatazo zitakaguliwa kwa kila mtu ambaye anaombwa kufanyiwa uchunguzi wa uhalifu, kwa kutumia alama za vidole kwa lazima kama ilivyoelezewa hapa chini:

1. Kituo cha Kitaifa cha Taarifa za Uhalifu (NCIC) Sajili ya Kitaifa ya Wahalifu wa Kingono na Shirika la Upelelezi la Shirikisho (FBI) hukagua alama za vidole kwa kutumia Utambuzi wa Kizazi Kipya.

2. Katika Jimbo ambalo mtu huyo anaishi: Sajili/ hifadhidata ya Unyanyasaji na Utelekezaji wa Watoto ya Jimbo, Ofisi ya Utambulisho ya Jimbo (SBI) au hifadhi ya uhalifu ya shirika lingine la Jimbo inayotumia alama za vidole, na Sajili ya Jimbo ya Wahalifu wa Kingono.

3. Katika kila Jimbo ambapo mtu binafsi ameishi kwa miaka mitano iliyopita: Sajili/hifadhidata ya Jimbo ya Unyanyasaji na Utelekezaji wa Watoto, SBI au hifadhi ya uhalifu ya shirika la Jimbo kwa kutumia au bila kutumia alama za vidole, na Sajili ya Jimbo ya Wahalifu wa Kingono.

**E. Mchakato unahitajika.** Mtu yeyote ambaye Mtoa Huduma ya Utunzaji wa Watoto anahitajika kuomba afanyiwe uchunguzi wa uhalifu lazima akubali kuchukuliwa alama za vidole. Polisi wa Jimbo watachukua (au kusimamia kuchukuliwa) kwa alama za vidole za mtu binafsi na watapeleka alama za vidole kwa Ofisi ya Jimbo ya Utambulisho ili kukagua sajili, hifadhi, na hifadhidata zinazohitajika zilizoorodheshwa hapa juu.

1. Idara itakapopokea ripoti ya historia ya uhalifu ya mtu huyo itafanya upekuzi wa hifadhidata ya Maine ya Unyanyasaji na Utelekezaji wa Watoto.

2. Ikihitajika, Idara itaomba kutafuta sajili, hifadhi na hifadhidata zote kwa kila Jimbo ambapo mtu huyo ameishi kwa miaka mitano iliyopita.

**F. Marudio.** Ukaguzi wa uhalifu lazima uombwe angalau mara moja kila baada ya miaka mitano kwa kila mtu anayehitaji ukaguzi wa uhalifu chini ya Sheria hii.

**G. Barua ya Ustahiki.** Idara itatoa matokeo ya uchunguzi wa uhalifu, kwa kutuma barua mbili, Barua ya Utunzaji wa Watoto ya Kustahiki ya Mtoa Huduma na Barua ya Mfanyakazi ya Kustahiki. Barua zote mbili zinatumwa moja kwa moja kwa mtu anayedhihirika kustahiki au kutostahiki ndani ya siku 45 za ombi lililowasilishwa.

**1.** Mfanyakazi mtarajiwa hawezi kuanza kufanya kazi kwa Mtoa Huduma ya Utunzaji wa Watoto hadi baada ya kumpa Mtoa Huduma ya Utunzaji wa Watoto Barua ya Kustahiki ambayo inaonyesha kuwa Mfanyakazi huyo anastahiki.

**2.** Wakati Idara imeomba upekuzi wa nje ya jimbo kwa mujibu wa 3(E)(2) ya sheria hii na bado haijapokea matokeo na imefikia siku 45 tangu ombi kuwasilishwa, Idara inaweza kutoa Barua ya Kustahiki kwa Mtoa Huduma ya Utunzaji wa Watoto kulingana na maelezo mengine yote yanayopatikana. Idara itatoa Barua ya Pili ya Mtoa Huduma ya Utunzaji wa Watoto ya Kustahiki na Barua ya Mfanyakazi ya Kustahiki ikiwa maelezo ya ziada kutoka kwa upekuzi wa nje ya jimbo yatabadilisha kustahiki kwa mtu huyo.

**H. Haki za Kukata Rufaa.** Ikiwa mtu hajastahiki kwa sababu ya matokeo ya ukaguzi wa historia, Barua ya Mfanyakazi ya Kustahiki itajumuisha msingi wa mtu huyo kutostahiki pamoja na taarifa kuhusu jinsi ya kukata rufaa matokeo haya kwa mujibu wa Sehemu ya 4 ya sheria hii.

**I. Faragha.** Matokeo ya ukaguzi wa uhalifu wa mtu binafsi hayatatolewa kwa umma au kusambazwa isipokuwa data haiwezi kumtambua na/au kujumuishwa na nyinginezo.

**J. Kutostahiki kwa Ajira.** Hali yoyote kati ya ziifuatazo inachukuliwa kuwa taarifa ya kutostahiki:

**1.** Kusajiliwa kwenye Sajili ya Jimbo au ya Kitaifa ya Wahalifu wa Kingono, au taarifa kwamba mtu huyo anahitajika kuorodheshwa kwenye sajili kama hiyo;

**2.** Uthibitisho wa Unyanyasaji au Utelekezaji wa Watoto unaofanywa na Idara, au Idara yoyote ya Jimbo inayolingana;

**3.** Hukumu ya makosa ya jinai kwa uhalifu wowote ufuatao:

**a.** Mauaji,

**b.** Unyanyasaji au Utelekezaji wa Watoto,

**c.** Uhalifu dhidi ya Watoto, ikiwa ni pamoja na ponografia ya Watoto,

**d.** Unyanyasaji wa wanandoa,

**e.** Uhalifu unaohusisha ubakaji au unyanyasaji wa kingono

**f.** Utekaji nyara,

**g.** Kuchoma mali,

**h.** Shambulio la kimwili/vurugu,

**i.** Kosa linalohusiana na dawa za kulevya lililofanywa katika miaka mitano iliyopita.

**4.** Kuhukumiwa kwa kosa la kikatili lililofanywa kama Mtu Mzima dhidi ya Mtoto, ikijumuisha unyanyasaji wa watoto, kuhatarisha watoto, unyanyasaji wa kingono, au kosa linalohusisha ponografia ya Watoto.

**5.** Kuhukumiwa kwa kosa, kama ilivyoainishwa na Idara, ndani ya miaka 10 iliyopita, ikijumuisha;

**a.** Mwenendo wa kutojali

**b.** Vurugu za unyanyasaji wa nyumbani

**c.** Unyanyasaji wa nyumbani unaotisha

**d.** Unyemeleaji wa unyanyasaji nyumbani

**e.** Mashambulizi

**f.** Mashambulizi wakati wa kuwinda

**g.** Vurugu za nyumbani zinaotishia kufanya uhalifu

**h.** Tabia ya kutojali ya vurugu ya nyumbani

**6.** Mtu ataamuliwa kuwa hastahiki ikiwa atakataa kufanyiwa uchunguzi wa kina au akitoa taarifa za uongo kwa maksudi kuhusiana na kufanyiwa uchunguzi wa kina.

**K.** **Wajibu wa Mtoa Huduma ya Utunzaji wa Watoto.** Hakuna Mtoa Huduma wa Utunzaji wa Watoto atakayeajiri Mhudumu ambaye hajawasilisha Barua ya Kustahiki kwa Mtoa Huduma wa Utunzaji wa Watoto inayoonyesha kuwa Mhudumu wa Utunzaji wa Watoto anastahiki, wala kumruhusu mtu yeyote anayejulikana na Mtoa Huduma wa Utunzaji wa Watoto kuwa hastahiki chini ya Sheria hii kuweza kumfikia Mtoto yeyote katika utunzaji wa Mtoa Huduma wa Utunzaji wa Watoto.

**L.** **Kukatazwa Leseni.** Taarifa za kutostahiki zikipatikana katika sajili, hifadhi na hifadhidata zozote zinazohitajika kwa uchunguzi wa kina wa Mtoa Huduma wa Utunzaji wa Watoto, au Mwanafamilia au ikiwa Mtoa Huduma wa Utunzaji wa Watoto au Mwanafamilia aliye katika Familia Inayotoa Huduma za Utunzaji wa Watoto haruhusiwi vinginevyo kwa sababu ya amekataa kuridhia kufanyiwa uchunguzi wa kina, au akitoa taarifa za uongo kwa maksudi kuhusiana na ukaguzi wa usuli, hakuna Leseni itakayotolewa kwa Mtoa Huduma huyo wa Utunzaji wa Watoto.

**M.** **Uchunguzi wa historia wa hiari.** Idara inaweza kuomba kwa hiari yake kwamba Mtoa Huduma ya Utunzaji wa Watoto, Mfanyakazi, au Mwanafamilia atie saini kutolewa kuidhinisha mamlaka ya Idara kufanya ukaguzi wa uhalifu kwa Ofisi ya Utambulisho ya Jimbo (SBI), hifadhidata ya unyanyasaji na kutelekezwa kwa watoto ya jimbo, na sajili ya jimbo ya wakosaji wa kingono. Matokeo ya ukaguzi wa hiari wa jina na tarehe ya kuzaliwa yanategemea masharti yote ya sheria hii, ikijumuisha kifungu cha 3(J)(1)-(6) na kifungu cha 4 cha sheria hii.

## SEHEMU YA 4. MCHAKATO WA RUFAA NA HAKI

A. **Usahihi Halisi wa Taarifa.** Mtu ambaye amebainika kutostahiki kwa sababu ya taarifa za kutostahiki zinazopatikana katika mojawapo ya sajili, hifadhi, na/au hifadhidata zilizokaguliwa na ambaye anapinga usahihi wa kweli wa taarifa za kutostahiki anaweza kuomba ukaguzi wa taarifa za kutostahiki moja kwa moja kwa wakala anayehifadhi sajili, hifadhi au hifadhidata hiyo. Maelekezo ya jinsi ya kupinga usahihi hali wa ripoti yatajumuishwa katika barua ya kushiriki matokeo ya uchunguzi wa uhalifu na mtu binafsi.

B. **Uthibitishaji wa Unyanyasaji au Utelekezaji wa Watoto.** Watu wanaopokea barua ya kutostahiki kwa sababu ya matokeo *yaliyothibitishwa wanaweza kuomba rufaa kwa mujibu wa Kanuni za Maine za 10-148 Sura ya 201 Kanuni za Taratibu za Mchakato wa Kuthibitisha Unyanyasaji au Utelekezaji, kwa Rufaa za Watu Waliothibitishwa kuwa Watendaji wa Unyanyasaji au Utelekezaji wa Watoto na Rufaa za Kukataa Ufikiaji wa Rekodi za Siri.*

   1. Mtu binafsi anaweza kuomba rufaa ikiwa mtu huyo hajaomba au kupokea rufaa awali.

      a. Ombi la rufaa lazima litumwe ndani ya siku 30;

      b. Minghairi ya sharti la siku 30 inatumika kwa hali fulani ambapo ugunduzi ulifanywa kabla ya tarehe 1/11/03 (tazama ukurasa wa 19 wa sheria, Sehemu ya XIV(B)) na matokeo ambayo yanastahiki kuzingatiwa upya chini ya Sehemu ya XV ya sheria (ukurasa wa 20);

      c. Mtu aliyethibitishwa ambaye anastahiki rufaa anapaswa kuwasilisha taarifa yoyote anayotaka mkaguzi awe nayo anapozingatia kama ugunduzi ulikuwa na msingi au la;

      d. Mchakato wa rufaa una hatua mbili, kwanza ni ukaguzi wa hati ambapo mfanyakazi maalumu wa Idara hukagua rekodi zote za Idara kuhusu ugunduzi pamoja na hoja yoyote iliyowasilishwa na mgunduzi wa rufaa na huamua ikiwa ugunduzi huo umethibitishwa au kubatilishwa;

      e. Ikiwa matokeo yatathibitishwa, mkata rufaa ana haki ya kuomba Kikao cha Usikilizaji wa Kiutawala kwa mujibu wa Kichwa cha 5: Taratibu na Huduma za Utawala Sura ya 375: Sheria ya Utaratibu wa Kiutawala wa Maine.

C. **Kuhukumiwa kwa sababu ya kosa.** Mtu ambaye alipokea Barua ya Wafanyakazi ya Ustahiki ya kutostahiki kwa sababu ya hukumu ya kosa, kama ilivyoainishwa na Idara katika Sehemu ya 3(J)(5) ya sheria hii ndani ya miaka 10 iliyopita anaweza kuomba rufaa ya kutostahiki.

   1. Ombi lililoandikwa la rufaa lazima litumwe ndani ya siku 30 baada ya tarehe ambayo Barua ya Mhudumu ya Kustahiki ilitolewa na linajumuisha;

      a. Hati zinazoonyesha kwamba hukumu ya makosa ndani ya miaka 10 iliyopita ndiyo matokeo pekee ya kutostahiki katika ukaguzi wa kina wa historia na;

      b. Hati zinazoonyesha kuwa hakujakuwa na hukumu za ziada za jinai za aina yoyote kufuatia hukumu ya kutostahiki na;

      c. Hati zinazoonyesha kwamba mtu huyo hayuko tena chini ya adhabu au masharti yoyote ya mfumo wa mahakama. Hii inaweza kujumuisha, lakini si tu, kipindi cha uangalizi.

**2.** Idara itakagua hati zote zilizowasilishwa ndani ya siku 10 baada ya kupokea hati.

**a.** Wakati vigezo vya 4(C)(1)(a) -(c) vimetimizwa, Idara itabatilisha uamuzi usiostahiki na kumpa mtu husika taarifa ya uamuzi na Barua ya Kustahiki kwa Wafanyakazi iliyosasishwa itatumwa kwa posta.

**b.** Wakati mtu huyo ameshindwa kutoa ombi la rufaa kwa wakati unaofaa au hajatoa hati za kutosha za vigezo vya 4(C)(1)(a)-(c) Idara itampa mtu huyo taarifa ya uamuzi kwamba hali ya kustahiki haijabadilika na itatoa maelekezo kuhusu haki ya mtu huyo ya kuomba Kikao cha Kusikilizwa cha Kiutawala kwa mujibu wa Kichwa cha 5: Taratibu na Huduma za Utawala Sura ya 375: Sheria ya Utaratibu wa Kiutawala wa Maine.

MAMLAKA YA KISHERIA**:** 22 M.R.S. §§ 42(1) NA 8302-A(1)(J),(2)(K).

HISTORIA: 25 SEPTEMBA, 2020 (KUPITISHWA KWA DHARURA)
SEPTEMBER 17, 2021 (KUPITISHWA KWA MUDA)
APRILI 12, 2022 (KUPITISHWA KWA MWISHO)